# AckySHINE.com

# Mungu ni nani? Sifa za Mungu

By DIN - Melkisedeck Leon Shine · May 2, 2015

Mafundisho ya Msingi ya Kanisa Katoliki: Makala za Katoliki · #Karibu AckySHINE · #Katoliki: Mungu

Mungu ndiye Muumba wa vitu vyote, katika mbingu na nchi, Mkubwa wa Ulimwengu mwenye kuwtunza watu wema na kuwaadhibu watu wabaya. (Mt: 6:8-9, Yoh 20: 17)

Sifa za Mungu

Mungu ni Muumba wa vitu vyoteMungu ni Muumba wa vyote maana yake amefanya vitu vyote kwa kutaka tuu pasipokutumia kitu chochote (Yoh. 1:3)

Mungu ni RohoMungu ni Roho kamili na ukamilifu wake hauna mpaka na haonekani wala hashikiki. (Yoh. 4:24, Kut 3:13-15, Zb 144:3, Lk: 24:39)

Mungu ni muweza wa yoteMungu anaweza kufanya kila anachokitaka. (Zab. 135:6)

Mungu ni wa MileleHii ina maana Mungu hana mwanzo wala mwisho, amekuwepo kabla ya nyakati, yupo na atakuwepo baada ya nyakati. Yeye ndiye anazifanya nyakati, Yupo daima. (1 Tim, 1:17)

Mungu ni mwemaMaana yake anavipenda na kuvitunza viumbe vyake hasa wanadamu na anavitakia mema tuu (Zab: 25:8-10)

Mungu ni mwenye hakiKila mtu hupata kwa Mungu Haki yake kadiri na anavyostahili.

Mungu aenea pote

Hii ina maana yupo kila mahali Mbinguni na Duniani, Hakuna mahalia asipokuwepo. (Zab: 139:7-12).

Mungu anajua kila kitu

Mungu anajua yote, ya sasa, ya zamani na ya wakati ujao hata mawazo yetu

Mungu ni mwenye hurumaAnawasamehe watu dhambi zao wakitubu

Mungu ni mwenye subira

Mungu anakawia kuwaadhibu wakosefu maana anataka kuwapa nafasi ya kuongoka. (Eze; 33:11, Zb: 102: 1-5)

Aidha Mungu yupo Mmoja tuu ambayae kwake kuna nafsi Tatu ambazo ni sawa, Baba ni Mungu, Mwana ni Mungu na Roho Mtakatifu ni Mungu. Hli ndilo linaitwa Fumbo la Utatu Mtakatifu. (Lk. 3:21-22)